# Faida za Utumizi wa Ramani ya Dhana katika Kufundishia Msamiati wa Kiswahili Shule za Msingi

Tumaini Samweli Mugaya
Chuo Kikuu cha Dodoma
samwelikebara@yahoo.co.uk

**MAKALA HALISI**

**HISTORIA YA MAKALA**

**Kupokelewa:** 20 Julai 2021

**Kurekebishwa:** 15Sept. 2021

**Kukubaliwa:** 29 Oktoba 2021

**Kuchapishwa:** 08 Dis. 2021

ISSN: 2453 – 6016

Juzuu 7,

Toleo 2,

pp. 29 – 42.

**NUKUU:** Mugaya, T. S. (2021). Faida za Utumizi wa Ramani ya Dhana katika Kufundishia Msamiati wa Kiswahili Shule za Msingi. *Ruaha Journal of Arts and Social Sciences*, *7*(2), 29 – 42.

**Ikisiri**

Makala hii imechunguza kuhusu faida za utumizi wa ramani ya dhana katika kufundishia kiswahili shule za msingi mkoani Dodoma. Mbinu za usaili na ushuhudiaji zimetumika kupata data za msingi. Data za msingi zilichambuliwa kwa kutumia mkabala wa Kitaamuli. Nadharia ya Ujenzi wa Maana ya Vygotsky imetumika katika kujadili masuala mbalimbali na kutoa picha halisi ya faida za utumiaji wa ramani ya dhana katika ufundishaji wa msamiati. Matokeo ya makala hii yameonesha kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya matumizi ya ramani ya dhana na ufundishaji wa misamiati ya lugha. Baadhi ya faida za kutumia ramani ya dhana kutafuatia maarifa ya awali ya mwanafunzi ni kupata maarifa ya maana elekezi, kutathmini kiwango cha uelewa wa mwanafunzi, kuwezesha utungaji wa msamiati, kujenga tajiriba ya kujieleza wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa msamiati na kutumika kama zana ya kufundishia na kujifunzia. Makala hii inapendekeza kuwa ramani ya dhana ni mbinu bora si tu inajenga uwezo mkubwa kwa wanafunzi katika kujifunza msamiati wa Kiswahili, bali ni mbinu yenye ufanisi mkubwa wa kutolea maarifa katika ufundishaji wowote.

**Maneno Msingi:** Lugha, Msamiati, Ramani ya Dhana na Kiswahili.

## Utangulizi

Kila jamii ina lugha mahsusi inayoitumia katika mawasiliano yake ya kila siku. Lugha huelezea mambo muhimu katika maisha ya kila siku na ndio hutambulisha uwepo wa jamii husika (Msanjila, 1990). Dhana hii huendana na ukweli kuwa baadhi ya misamiati ya lugha hunasibishwa na majina ya jamii na mahali. Ufundishaji wa misamiati ya lugha ni suala muhimu katika matumizi mapana ya kijamii na yale ya kitaifa yanayolenga kutolea maarifa. Msamiati ndio msingi wa maarifa ya lugha yoyote (Tarkashvand, 2015). Kabla mwanafunzi hajaanza kujifunza stadi za lugha yoyote, hana budi kujifunza na kumudu msamiati wa lugha hiyo. Kiswahili ndiyo lugha ya kufundishia nchini Tanzania. Kumudu misamiati ya lugha hii kutasaidia

kujenga uelewa na kuboresha mawasiliano darasani. Msamiati hujenga stadi za lugha za kusikiliza, kuongea, kusoma na kuandika.

Hapana shaka kuwa, licha ya lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia nchini Tanzania, bado hapajawa na ukomo wa mbinu mahsusi inayopaswa kutumika kufundishia misingi imara inayolenga kuikuza lugha hii katika viwango mbalimbali vya kielimu. Tafiti zinaonesha kuwa, mwanafunzi anapokuwa na misamiati ya kutosha katika lugha ya kufundishia, humsaidia kupata maarifa na kumuimarisha kutoka lugha ya awali isiyo rasmi (Ertürk, 2016; Richards et.al, 2001 & Banisaeidi, 2013). Ufanisi wa matumizi ya lugha kwa kiasi kikubwa hutegemea uwepo wa mbinu kadhaa za kufundishia.

Ramani ya dhana ni mbinu ambayo hutuelekeza kwenye wazo amilifu linaloweza kuelezewa kupitia nadharia ya utambuzi na ile ya ujenzi wa maana. Nadharia hizo huelezea ramani ya dhana kama mbinu muhimu ya kufundishia na kujifunzia darasani. Mbinu hii hutumika kuelezea somo, kuchanganua mada na kuendelezea fikra tunduizi katika ujifunzaji. Utumizi wa ramani ya dhana katika ufundishaji na ujifunzaji ulianza kuendelezwa na Gowin (1984) akiegemea katika kazi za Ausubel (1963) ambazo zimekuwa zikibainisha matumizi ya ramani ya dhana katika uga wa elimu kama mbinu za kisasa. Matumizi ya ramani ya dhana katika ujifunzaji na ufundishaji humshughulisha mwanafunzi kuwa na uwezo wa vipengele fulani katika ujifunzaji wa lugha akitofautisha dhana mbalimbali na kuunda dhana kuu moja kabla ya kuanza kujifunza na kubainisha maarifa mapya (Ausubel, 2000). Mbinu hii humsaidia mwalimu kutoa mwongozo, kuchochea, kumotisha, kutathmini ya utendaji, kuhifadhi na uhawilisho wa maarifa darasani.

Graves (2006) anasema kuwa ramani ya dhana ni michoro inayoonesha grafu za habari zinazohusisha mada na mada na kuchochea maana ya maneno yanayohusiana. Mwalimu na mwanafunzi wakishirikiana kujenga mchoro wenye misamiati inayohusiana katika kujenga somo au habari ama wazo kuu moja, huwafanya kujenga maarifa kwa urahisi. Hali hii huwasaidia wanafunzi kuongeza msamiati kutoka maneno wanayoyafahamu na kupata msamiati mapya. Katika kujifunza msamiati mpya kunahitaji jitihada, upenzi wa lugha, umakini, hasa kwa watoto ambao njia hii itaonekana kuwa mpya kwao.Ramani ya dhana ni mbinu yenye uelekeo wa ujifunzaji unaoegemea kwa mwanafuzi. Mbinu ya ramani ya dhana imeonekana kuwa fanisi katika ufundishaji wa sayansi zaidi kuliko ufundishaji wa sanaa na kuonekana kutumika kwa kiwango kidogo katika kufundishia lugha hasa lugha ya Kiswahili. Pengine hii inatokana na ukweli kuwa, upo ufaulu mzuri wa wanafunzi wanaosoma masomo ya lugha kwa kutumia njia na mbinu zinginezo.

Zipo sababu za kuangalia msamiati wa lugha ya Kiswahili katika kujifunza. Soureshjani (2011) anabainisha sababu hizo kwa kuangalia msamiati wa lugha ya pili ama lugha ngeni kama kilivyo Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za msingi nchini Tanzania. Sababu hizo hutokana na ukweli kuwa kumwezesha mwanafunzi kujifunza msamiati ni kumfanya awe na uwezo wa kuielewa lugha kwa ufanisi. Kujifunza lugha

si sehemu ya kujifunza kuelewa msamiati wa lugha, bali ni kuboresha mawasiliano katika tendo la kufundisha na kujifunza ili kupata maarifa. Wazo hili limeshadidiwa vizuri na Richards na wenzake (2001) anayedai kuwa msamiati ndio kiini cha umahiri wa lugha na hutoa msingi kwa anayejifunza lugha ili aweze kuiongea, kuisikiliza, kuisoma na kuiandika. Hali hii ina maana kuwa wanafunzi watakapoielewa misamiati ya lugha ya Kiswahili vizuri watajengewa uwezo mkubwa wa uelewa wa lugha na kuitumia vizuri kama chombo cha mawasiliano katika masomo mengine. Sababu ya kujifunza msamiati wa lugha umeelezwa vizuri na (Laufer, 1997) kwamba kujifunza msamiati wa lugha ndio moyo wa lugha yoyote katika matumizi.

Msamiati ni kiungo muhimu cha ufafanuzi wa dhana zinazobeba mawazo mbalimbali wakati wa ufundishaji wa lugha kwa wanafunzi hasa wanapoanza kusoma. National Reading Panel (2001) wanaeleza kuwa ufundishaji msamiati ni muhimu kwa sababu maneno yote tunayoyajua katika uelewa wetu, huelezea mawazo yetu kwa namna tunavyoweza kujenga mawazo mapya. Misamiati ndio kitita kinachobeba hadithi, mawazo na maudhui ili kujenga maarifa kwa watoto. Maarifa katika maneno ya wanafunzi uhusishwa na mafanikio ya kitaaluma kwa sababu mwanafunzi anapokuwa na msamiati anaweza kupata mawazo mapya na dhana mpya zaidi kuliko mwanafunzi mwenye misamiati michache (Chall & Jacobs, 2003). Kwa mfano, Beck, McKeown & Kucan (2002) wanabainisha vikwazo vinavyoweza kutoendeleza misamiati ya lugha katika shule za msingi ambavyo ni wanafunzi kuwa na maarifa hafifu ya lugha husika. Hali hii hujitokeza pale wanafunzi wanapopimwa katika matumizi yao ya vitabu na wanapokuwa katika mazungumzo.

Wanazuoni wengi wa elimu wanakubaliana kuwa, ramani ya dhana humwezesha mwanafunzi kupata maarifa katika makundi yao ya rika, masomo mbalimbali na katika muktadha wa mazingira mbalimbali. Hali hii huwajengea uwezo wa kufikiri na kupata maarifa kwa kina wanaposhirikiana. Matumizi ya ramani ya dhana yamekuwa sio zoelefu katika matumizi ya ufundishaji na ujifunzaji nchini Tanzania. Makala hii inajaribu kuelezea ramani ya dhana kama mbinu muhimu ya ufundishaji na ujifunzaji ikijadili umuhimu wake katika ufundishaji na ukuzaji wa lugha ya Kiswahili.Mbinu inayoondoa ombwe la mchangamano wa mawasiliano kati ya watoto wa shule za msingi na watu wazima kama vile wazazi nyumbani na walimu shuleni. Hakuna shaka kuwa msamiati ni maneno yanayobeba maudhui mbalimbali yenye kubeba majina, viwakilishi, vivumishi, vielezi, vitenzi, vihisishi na viunganishi. Msamiati wa awali wa mwanafunzi huanza kwa kuelezea maneno ya aina hizo katika lugha ya Kiswahili.

**Mbinu na Nadharia ya Uchunguzi**

Makala hii imetumia mbinu ya kimaktaba na uwandani uwandani katika kupata data za msingi zilizowasilishwa kwa rejea. Usaili na ushuhudiaji ulitumika kupata data za awali. Mbinu ya uteuzi lengwa ilitumika kuwapata walimu wa mkoa wa Dodoma waliohojiwa wakiwakilisha wengine nchini. Uwasilishaji wa data ni wa kimaelezo ulio katika mwelekeo wa nadharia ya ujenzi wa maana unaomsisitiza mwanafunzi ashiriki kujenga maarifa yake. Kazi hii imesheheni mifano inayoonesha namna dhana

zinavyohusishwa katika michoro na kujenga wazo kuu moja ili kumpa mwanafunzi uwezo wa kubainisha mambo na kumpa uelewa wa kutosha wakati wa kujifunza.

Ramani ya dhana ni mlengo mojawapo wa nadharia ya ujenzi wa maana. Mwasisi wa nadharia hii ni Vygotsky.Mawazo makuu katika nadharia hii ni kwamba, mwanafunzi hujifunza lugha kutokana na mchangamano wa malezi anayoyapata katika mazingira yake na utamaduni ndio huunda maarifa ya mwanafunzi. Nadhari hii husisitiza ujenzi wa maana kwa mwanafunzi akiwa ndiye kitovu cha mwegamo wa maarifa. Suala la mtoto kupokea misamiati ni mchakato endelevu wa kila siku katika maisha yote ya binadamu. Mtoto huanza kujifunza msamiati kupitia maneno anayoyajua, kuyafahamu na anayoweza kuyatumia kwa ukamilifu na pale anapoendelea kujifunza hupata uzoefu mpya (Hart & Risley, 1995). Mtoto huanza kupokea na kujifunza lugha kutoka kwa wazazi wake nyumbani. Idadi ya msamiati huongeka kwa kadri inavyoisikia na kuitumia tangu ututoni akiwa nyumbani na kuendelea kujifunza akiwa shuleni na baadaye katika maisha yake yote.

Nadharia ya ujenzi wa maana imetumika kuongoza makala hii kuangalia misamiati kama sehemu ya lugha ambapo lugha ya Kiswahili ndiyo kitambulisho cha utamaduni kinachoakisi maisha halisi ya wanafunzi wengi wa kitanzania. Changamoto za kujifunza msamiati wa lugha ya Kiswahili wanazozipata wanafunzi baada ya kutoka nyumbani na kuingia shule za msingi, ndizo zilizoibua makala hii. Nadharia hii ya ujenzi wa maana imefaa kwa vile inayozingatia kuwa lugha na elimu hujengwa katika mchangamano wa kijamii unaozingatia mazingira, miiko na uzoefu wa maisha ya kila siku ya mwanafunzi (Irez & Han, 2011). Kazi hii inabainisha kuwa misamiati hujenga lugha na lugha hujenga maarifa.

**Faida za Kutumia Ramani ya Dhana katika Ufundishaji wa Msamiati**

Matokeo ya udurusu wa nyaraka, usaili na ushuhudiaji unaonesha kuwa, zipo faida kadhaa zilizobainishwa katika kazi hii ambazo ni matokeo ya utumiaji wa ramani ya dhana katika ufundishaji. Baadhi yake ni kutumia ramani ya dhana kutafuatia maarifa ya awali ya mwanafunzi, kupata maarifa ya maana elekezi, kutathimini kiwango cha uelewa wa mwanafunzi, kuwezesha utungaji wa msamiati na kujenga tajiriba ya kujieleza katika ufundishaji wa msamiati na kutumika kama zana ya kufundishia na kujifunzia. Faida hizi zimejadiliwa katika mada ndogo zifuatazo.

**Ramani ya Dhana Hutumika Kutafuatia Maarifa ya Awali**

Pale wanafunzi wanapojifunza msamiati wa lugha katika mfumo wa dhana hii, humrahisishia mwalimu kubaini maarifa ya mtoto ya awali katika dhana anazozifahamu na kuzitumia katika mfumo wa ramani ya dhana kama chombo cha kupimia maarifa (Birbili & Lin, 2001 & Cook, 2017). Katika usaili mwalimu mmoja alisema:

> Ufundishaji msamiati mpya huanza kwa mtoto kubunga bongo akitabiri maana ya neno alilopewa. Akishindwa husaidiwa kwa kuhusisha msamiati mpya na maneno mengine

> anayoyafahamu; kwa kuhusisha neno jipya na picha ili atabiri maana ama kuigiza atabiri neno katika mchoro (**Chanzo**: Data uwandani, 2021).

Nukuu hiyo inadhihirisha kuwa kujifunza msamiati au neno katika lugha si kumkaririsha mwanafunzi ili akumbuke bali ni kuweka neno au msamiati katika matumizi. Mfumo huu humruhusu mwanafunzi ajifunze kwa urahisi akijitegemea na pale anapopata maana halisi, hujenga maarifa ya kudumu kwa kadiri anavyopata msamiati mpya. Ramani ya dhana katika ufundishaji na ufundishaji hujenga msingi wa kiwango cha juu cha ufikirivu. Bila kuelewa dhana, hakuna ufahamu na maendeleo ya mtoto kiakili.

Tafiti zinaonesha kuwa, kila habari anayoipata mtoto katika kujifunza, huichakata na kuitunza ndani ya akili ya ubongo wake katika sehemu ya lugha ubongoni. Mchakato huo uhusisha uoni wa namna maarifa hayo yanavyoyahusishwa na mfumo wa kumbukumbu za kudumu zinazompatia maarifa ya kina. Ingawa mfumo wa ubongo huundwa kwa vipande vipande vidogo vyenye uwiano wa kifani, ramani ya dhana ni mbinu mojawapo inayotumika kama mfumo wa kidau kinachoandaa maarifa yenye dhana kadhaa zilizopandwa katika mfumo mahususi wa kujifunza.

Carrel na wenzake (1989) wanabainisha kuwa, ili mwanafunzi aweze kuitumia lugha katika utungaji, anatakiwa abunge bongo kuhusu wazo fulani la mada lengwa. Hali hii huanza na mpango wa kutafuta mawazo ya awali ya mwanafunzi aliyonayo akilini mwake kabla ya kutumia stadi za lugha. Hatua hii uhusisha kufikiria mada husika, kuhusisha mawazo yaliyobeba dhana mbalimbali, kuonesha mawazo hayo katika maandishi, ramani za michoro pia katika grafu za dhana. Watafiti wameonesha kuwa mpango wa maarifa ya awali katika ramani ya dhana sio tu humpa mwanafunzi uwezo wa kujenga dhana na msamiati katika habari, bali pia humpa mpango jumuifu wa dhana anazotakiwa kujifunza.


Ojima (2006) anaonesha kuwa mbinu ya ramani ya dhana ni mkakati faafu wa kufundishia uandishi katika mpango kazi wa kutafuta maarifa ya awali. Katika kazi yake aliangalia uhusiano wa maneno yaliyokuwa katika udarajia na kuyafundisha kwa vitendo na michoro bunilizi wakati wa kuanza mjadala wa awali wa somo. Mbinu hii ilionesha kuongeza ushiriki wa wanafunzi katika somo hasa walipoonekana kuwasiliana wao kwa wao na kutoa mawazo darasani. Utafiti wa Ojima uliendelea kuonesha kuwa mwalimu alipokuwa darasani na kuanza kutambulisha somo akielekeza misamiati ya mada ili wanafunzi waione ubaoni kwa kutumia michoro, wanafunzi waliongeza ushiriki katika majadala wa somo kwa namna ambayo iliwasaidia kupanua maana za msamiati iliyotambulishwa.

Nadharia ya ujenzi wa maana ambayo ni nadharia ya usasa katika elimu humwona mwalimu wa lugha kama mfunzaji, mwezeshaji wa maarifa na mjenzi wa mazingira ya ufundishaji (Jia, 2010 & Darmofal na wenzake, 2002). Darmofal na wenzake (2002) wanabainisha kuwa kujifunza ni kujenga dhana zinazomwezesha mwanafunzi

kujenga maarifa yake mwenyewe kutokana na maarifa yake ya awali aliyonayo kutokana na uzoefu wake wa kila siku. Kadri mwanafunzi anavyotumia misamiati kujenga hoja, ndivyo anapoitumia lugha na kupata maarifa.

**Ramani ya Dhana Huwezesha Kupata Maarifa ya Maana Elekezi ya Msamiati**

Matumizi ya ramani ya dhana hupangilia mawazo kwa namna inayojenga mantiki elekezi. Katika njia za usaili kwa walimu, ushuhudiaji darasani na udurusu wa nyaraka zilitumika ili kubaini miundo ya ramani ya dhana. Matokeo yalionesha kuwa ramani ya dhana zilitumiwa na walimu katika miundo kadhaa kulingana na wazo lililoabiliwa pia uhuru aliokuwa nao mwanafunzi kulingana na ubunifu wake unaomjengea maana kwa urahisi kutokana na mazingira yake ya kila siku. Hali hii ilisaidia kutoa maana elekezi. Michoro ifuatayo ni baadhi ya miundo ya ramani za dhana iliyoshudiwa kutumika darasani kuonesha maana elekezi kuwa wazazi ni dhana inayohusisha baba na mama.





**Chanzo:** Data uwandani (2021)

Katika kazi za michoro ya namna hiyo, husaidia wanafunzi kufanya fikira tunduizi za kina pale wanapopangilia dhana walizopewa ili kujenga wazo kuu moja. Tamani ya dhana huwezesha fikra bunifu katika muundo wa kidarajia ambao hudhihirika kwa mpangilio wa michoro yenye vijenzi elekezi (Novak na mwenzake, 2006). Katika mchoro husika kila dhana inaunganishwa na dhana nyingine ili kujenga maana ya dhana zote. Dhana hizo ni lazima ziungane ili kujenga dhana kuu moja ya msingi. Wanafunzi wanapoangalia ramani za dhana walizoziunda huweza kuonesha uhusiano wake kuelekea dhana kuu (Afamasaga-Fuata'i, 2009). Uunganishaji wa dhana husaidia kupangilia mawazo kwa urahisi, kuunda maarifa mapya na uelewa ilhali wakihakiki fikra zao na kuongeza uelewa wa miundo ya dhana za mada husika na kutoa tafsiri mbalimbali zenye mawazo mapya ya mada husika. Mwanafunzi hufanya urejeshi husishi ambao hujenga maarifa ya kudumu kwa kutumia misamiati ya lugha iliyojengwa katika mfumo wa ramani ya dhana.

**Ramani ya Dhana Hutathmini Kiwango cha Msamiati wa Mwanafunzi**

Kipengele hiki kidogo kinatuelekeza kuwa, ramani ya dhana ni kipimo cha kutathmini msamiati wa lugha kwa mwanafunzi. Tathmini hufanyika pale anapojenga hoja kwa kazi mbalimbali anazopewa darasani tafakari. Wanafunzi wakipewa maneno kama (kuku, matunda, mayai, embe, chakula na ndizi) kisha wakabadilishana ramani ya dhana walizoziunda darasani. Wakachangia mawazo kwa kuboresha msamiati ya

maneno mengine waliyoyapata kutokana na ujenzi wa uelewa wao kama ilivyo katika michoro, hali hii husaidia kufanya tathmini.





**Chanzo:** Data uwandani (2021).


Mwanafunzi akipewa dhana zinazompa tafakari tunduizi, kazi hizo humjengea mwanafunzi uwezo wa kujitathmini mwenyewe anapoitumia lugha na matokeo yake humjengea maarifa. Kwa namna hii ramani ya dhana hupima kiwango cha msamiati katika lugha na maendeleo ya mwanafunzi kwa namna anavyopokea maarifa aliyoyapata (Wheeler & Collins, 2003). Ramani ya dhana ni nyenzo muhimu ya kuona namna mwanafunzi anavyodhihirisha maarifa, anavyowaza, anavyojieleza katika kulielewa somo na kupima makuzi yake katika tendo la kujifunza. Akinsanya na wenzake (2004) wanasema kuwa ramani ya dhana hukuza uwezo wa akili katika kuchanganua na kubainisha mambo na kuondoa dhana potofu katika ujenzi wa maarifa (Gul & Boman, 2006).

Kathol na wenzake (1998) wanashuhudia kuwa ramani ya dhana hupima maarifa ya mwanafunzi kwa wakati huo huo na kutoa fursa ya kuendelea na hatua zingine katika maendeleo yake anapojifunza. Mwanafunzi asipoelewa msamiati unaobeba wazo fulani kuu ni vigumu kuendeleza wazo hilo na kuelewa ujenzi wa dhana kuu inayoelekezwa. Wanafunzi wanaweza kujenga ramani ya dhana kwa kutumia namba, udarajia pia uhusiano kwa kupangilia mwingiliano wa dhana husika. King na mwenzake (2002) wanabainisha kuwa ramani ya dhana hupima maarifa mtoto, ubunifu na uhuru wa utendaji katika viwango vyote vya elimu. Eppler (2006) anasema kuwa ramani ya dhana hupima uwezo wa lugha na maarifa ya awali ya mwanafunzi na zaidi ya hapo hupima mada zilizopita.


**Ramani ya Dhana Huwezesha Utungaji wa Msamiati**

Matumizi ya ramani ya dhana katika hatua ufahamu na utungaji wa msamiati huwa na matokeo chanya katika kazi za mwanafunzi kwa namna kadhaa. Mfano namba 1 unaonesha mishale inayoelekeza na kumfanya mwanafunzi aweze kufanya utungaji kuwa, matokeo ya familia ya baba na mama ni watoto na mfano namba 2 ni mchoro unaoonesha duara moja lenye vipande vinne vyenye rangi tofauti vinavyounda kitu kimoja yaani vitu vinne vikiunganishwa huunda kitu kimoja kama ilivyo katika kuandika robo ya duara moja katika mada hiyo ya darasa la kwanza.







Ukitengeneza ramani ya dhana na kuacha sehemu zingine ili wanafunzi wajaze wenyewe kutoka kwenye dhana au kifungu cha habari ulichowapa, huwawezesha kufanya utungaji wa msamiati. Mfano katika kielelezo kifuatacho unaweza kumwelekeza mwanafunzi aseme kuwa Matunda na kuku ni vyakula.




**Chanzo:** Data uwandani (2021)

Namna nyingine ni kuwaelekeza wanafunzi waandike maneno ya msingi katika ramani ya dhana, kisha waombe wanafunzi wajaze kila sehemu ya nafasi ya iliyoachwa wazi. Waombe waandike au wasema neno la msingi linalobeba dhana zingine zitakazoachwa. Namna hii huwawezesha kufanya utungaji wa msamiati.




**Chanzo:** Data uwandani (2021)


Utungaji husisimua ubunifu, huchangamsha maarifa ya mwanafunzi, huandaa mawazo ya wanafunzi katika kukabiri kazi zilizopangwa mapema, hutoa hitimisho yakinifu la maudhui, hupima utayari wao katika kazi wakati wa kujifunza, huamasisha mchangamano na wengine, hujenga ubora katika matumizi fanisi ya lugha. Ushahidi katika hili ni pale mwalimu anapochokonoa wazo kwa kutumia msamiati ili wanafunzi watoe uelewa wao. Kwa mfano, Dyer's (1985) alifanya utafiti na kutaka kujua kama ramani ya dhana ilikuwa na faida kwa usomaji wa hadithi. Matokeo yalionesha kuwa wanafunzi waliotumia ramani ya dhana walibainisha mawazo yao vizuri katika ufahamu wa misamiati ya somo na walifaulu vizuri zaidi katika utungaji kwa kupata alama za juu kuliko wale ambao hawakutumia ramani ya dhana. Liu Chen na Chang (2010) katika utafiti wao umeonesha kuwa ramani ya dhana ilikuwa ni kisaidizi cha mfumo wa kikompyuta katika kujifunza kusoma lugha ya pili ya Kingereza kama lugha ya kigeni nchini China. Ramani ya dhana inaweza kutumika kufundishia msamiati wa Kiswahili kikiwa ni lugha ya pili ya mwanafunzi wa shule ya msingi ns mbadala kutoka lugha ya mama.

**Ramani ya Dhana Hujenga Tajiriba katika Maelezo ya Kufundishia Msamiati**

Ramani ya dhana haimzuii mwanafunzi kuacha kufikiri na kuitumia tu kama zana ya kujifunzia bali hutumika kama zana ya kujengea hoja na kuwasilisha maarifa pale wanafunzi wanaposhiriki kutoa mawazo waliyonayo katika mada iliyotolewa ili

kujenga picha ya pamoja katika kushiriki kwa pamoja ili kujenga maarifa. Hii ina maana kuwa ramani kama zana hutoa muktadha huru wenye mawanda mapana ya ushiriki hasa mwanafunzi anapotumia msamiati ili kuimudu lugha na kuongeza maarifa.

Pale wanafunzi wanapojiundia maana zao wenyewe ili kujenga uelewa wa dhana mbalimbali na uhusiano wake, dhana hizo huwajengea tajiriba katika ueledi wa misamiati. Mchoro unaofuata unaonesha mwanafunzi wa darasa la tatu akitumia dhana kuu ya *'kutoa'* kwa kupangilia tarakimu kwa muundo wa wima ili apate jibu wakati mwalimu akiweka rekodi.




**Chanzo:** Data uwandani (2021)

Wakati wanafunzi wanapojadili misamiati mipya, ramani ya dhana huwasaidia kuhusisha dhana mpya katika mada mpya wakijieleza vizuri. Matokeo yake hujenga ushiriki wenye mawasiliano huru wakichunguza namna wanavyojenga tungo zao, wakisemezana na kuhakiki hoja pia kuzitafakari wazi miongoni mwao. Hali hii hujenga mrejesho na kufanya udurufu wa yale waliyojifunza katika mada mbalimbali. Njia hii ni shirikishi inayowajengea walimu na wanafunzi kujiamini pale wanapotoa maelezo juu ya mada walizozianda ili kuchangamana katika tendo la kujifunza (Wheeler & Collins, 2009) kwa sababu huwaondolea wote uoga, wasiwasi na kuwajengea motisha katika kujieleza (Beitz, 1998).

Ertürk (2016) anabainisha kuwa pale ambapo ujifunzaji wa lugha utakapoambatana na matendo ya mbinu kadhaa, wanafunzi hujenga uelewa mkubwa. Matumizi ya ramani ya dhana kama yanavyobainishwa katika makala hii yanaweza kumwingiza mwanafunzi katika tajiriba ya utendaji inayoimarisha lugha ili kujenga uelewa. Mtazamo wa awali wa ufundishaji msamiati kijadi ulionekana kupitwa na wakati kwa vile kuchosha wanafuzi. Hali hii ilitokana na ukweli kwamba mtazamo wa kijadi ulilenga kukaririsha msamiati tofauti na mtaala wa shule za msingi unaoelekeza kumjengea mtoto uwezo wa kujifunza msamiati kwa uelewa. Mwalimu mmoja alipoulizwa kuhusu tatizo la kukariri msamiati kwa mbinu za kijadi katika ufundishaji wake wa Kiswahili alisema:

> Wanafunzi wangu wa darasa la kwanza wanapata shida ya kuelewa somo wakati wa ufundishaji na katika vitabu vyao. Hawaelewi maneno mengi na ukiyafundisha hawayakumbuki.

> Pia, wakiwa wenyewe hutumia lugha zisizo rasmi. Ninapojaribu kuwasaidia ninashindwa maana sina kamusi ya Kiswahili (**Chanzo:** Data uwandani, 2021).

Matumizi ya ubaoni tu au kifungu cha habari katika kitabu havitoshelezi na humfanya mwanafunzi kusahau kwa wepesi na kupoteza maana na hivyo lipo hitaji la mbinu mbadala. Zipo njia kadhaa zinazobainisha maana ya msamiati. Ramani ya dhana ni mbinu huru na wazi ambayo inahusisha kuonesha vitu halisi, kutoa maelezo, hisia, matendo halisi, michoro, tafsiri na kumjengea mwanafunzi tajiriba (AL Qahtani, 2015). Mbinu hii inafananishwa na kifaa cha kufundishia kinachojenga maarifa kwa namna ambayo mwalimu akikitumia huweza kuhusisha dhana katika zana huku akitoa maelezo yanayomjengea mwanafunzi maana.

Nadharia ya ujenzi wa maana huiangalia misamiati ya lugha kama vijenzi muhimu vya lugha na vijenzi wa hoja mbalimbali. Makala hii inajaribu kuonesha kuwa ufundishaji wa msamiati huleta ufanisi ufuatao; kujenga uongeaji wa mfululizo, kujenga tajiriba katika stadi za lugha, kumfundisha mtu maneno mapya, kutoa mikakati ya kujifunzia maneno na kujenga urazini katika maneno. Graves (2006) anasema kuwa msamiati ukitumiwa katika matendo na kazi mbalimbali humsaidia mwalimu aweze kuelekeza wanafunzi waunde msamiati kwa ufanisi wa kuitumia lugha kwa uwazi katika shule za msingi.

**Matumizi ya Ramani ya Dhana katika Uga wa Elimu**

Ramani za dhana ni mbinu muhimu za kutolea maarifa na kufanya tathmini wakati wa ufundishaji na ujifunzaji darasani. Mbinu hii hulenga kumwezesha mwanafunzi aweze kujifunza kwa urahisi akiwa chanzo cha maarifa na kujenga maana mwenyewe. Maarifa ni kitu kinachojengwa katika mchangamano wa kijamii hivyo mwalimu ataoe maarifa katika mchangamano unaomwegemea mwanafunzi zaidi na yeye awe ni mwezeshaji wa maarifa (Brown, 2007). Michoro ya ramani za dhana hutumika kufundishia sarufi ya lugha ikipima stadi za lugha za kusikia, kuzungumza, kusoma na kuandika. Hali hii huwahusisha zaidi wanafunzi ili wajenge usikivu na kuwa sehemu ya ujenzi wa maarifa wanayoyapata kwa namna mbalimbali. Pale wanapotumia michoro, grafu na kuunganisha na dhana walizopewa, huwafanya wafikiri na namna tunduizi na kuwahusisha katika kufikiri kwa kina ili watatue masuala ya dhana walizopewa katika somo kama sehemu ya jamii wanayoishi.

Ramani ya dhana hutoa fursa ya mazungumzo ili wanafunzi washiriki kutoa mawazo yao katika somo. Hali hii huwaendeleza kijamii na kiakili hasa pale wanapounda neno, maneno na tungo ili wajieleze au wanapopewa misamiati ili waweze kuibaini katika kifungu cha habari walichopewa. Matokeo yake hujenga udadisi na ubunifu katika tendo la kujifunza. Ramani ya dhana hutumika kama nyenzo ya kufundishia na kujifunzia ikienda sanjari na tathmini ya maarifa. Wanafunzi wanapopewa dhana mbalimbali ili wazihusishe na kuzipanga kidarajia katika mfumo wa mchoro ya ramani ya dhana ili ilete maana ni nyenzo muhimu katika kujifunza. Pale mwanafunzi anapopanga dhana alizopewa ili atengeneze wazo kuu mmoja husababisha ajenge

ubunifu mkubwa na kumfanya ajipime yeye mwenyewe kabla na baada ya mwalimu kumfanyia tathmini. Matokeo yake hujenga usikivu, ushiriki na kupima maarifa kwa wote. Ieleweke kuwa matumizi ya ramani ya dhana yatakuwa yenye tija pale mwalimu atakapofanya maandalizi ya kina, atakapojenga mazingira rafiki na shirikishi katika kujifunza, kupangilia muda vizuri ili aweze kukamilisha maudhui lengwa.

**Hitimisho**

Makala hii imebainisha mambo muhimu ya kutumia ramani ya dhana katika kufundishia misamiati ya lugha kwa watoto wa shule za msingi. Imeonesha kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya ramani ya dhana na uendelezaji wa lugha. Mwanafunzi anapotumia ramani ya dhana katika kujifunza msamiati wa lugha ya Kiswahili, hupata matokeo makubwa yenye kumpa uwezo wa kuitumia lugha vizuri katika kuwasiliana na kupata maarifa katika masomo yote. Bado Kiswahili ndiyo lugha pekee ambayo matumizi yake yameenea katika mfumo rasmi wa shule za msingi na mfumo usiyo rasmi. Licha ya kuwapo kwa changamoto za ufundishaji katika somo hili, bado walimu wanahitaji mbinu mwafaka za ufundishaji msamiati na uendelezaji wa lugha ya Kiswahili.

**Marejeleo**


Afamasaga-Fuata'i, K. (2009). *Concept Mapping in Mathematics: Research into Practice.* New York: Springer.

Akinsanya, C., & Williams, M. (2004). Concept Mapping for Meaningful Learning. *Nurse Education Today, 24*(1), 41-46.

AL Qahtani, M. (2015). The Importance of Vocabulary in Language Learning and How to Be Taught. International Journal of Teaching and Education, 3(3), 21-34.

Ausubel, D. P. (1963). The Psychology of Meaningful Verbal Learning. New York: Grune & Stratton.

Ausubel's. D. P. (1968) Assimilation Theory, Has Proposed the Rules for the Construction of Concept Maps.

Ausubel, D. P., Novak, J. D., & Hanesian, H. (1986). Educational Psychology: A Cognitive View (2nd Ed.). New York: Werbel And Peck.

Ausubel, D. P. (2000). The Acquisition and Retention of Knowledge: A Cognitive View. Boston, MA: Kluwer.

Banisaeid, M. (2013). Comparative Effect of Memory and Cognitive Strategies Training on EFL Intermediate Learners' Vocabulary Learning. English Language Teaching, 108 - 118.

Beitz, J.M. (1998). Concept Mapping. Navigating the Learning Process. *Nurse Educator, 23*, 35–41.

Beck, I. L., Mckeown, M.G., & Kucan, L. (2002). Bringing Words to Life: Robust Vocabulary Instruction. New York: Guilford Press.

Beitz, J.M. (1998). Concept Mapping. Navigating The Learning Process. *Nurse Educator, 23*, 35–41.

Birbili, M. (2007). Mapping Knowledge: Concept Maps in Early Childhood Education. Retrieved August 4, 2010, From Http://Ecrp.Uiuc.Edu/V8n2/Birbili.Html.

Birbili, M., & Lin, H. (2001). Mapping Knowledge: Concept Maps in Early Childhood Education. *Journal of Interactive Learning Research*, 8(3-4), 289-308.

Brightman, J. (2003). *Mapping Methods for Qualitative Data Structuring (QDS).* Paper Presented at Conference Of Strategies in Qualitative Research: Methodological Issues and Practices Using QSR Nvivo and NUD*IST. Institute of Education, London. 8-9 May 2003.

Brown, D. H. (2007). *Principles of Language Learning and Teaching.* Pearson Education, Inc.

Brown, D. H. (2014). Princilpes of Language Learning and Teaching; A Course in Second Language Acquisition. New York: Pearson Education.

Chall, J. S.,& Jacobs, V. A. (2003). Poor Children's Fourth-Grade Slump. American Educator, Spring, 2003. American Federation of Teachers.

Carrell, P. L., Pharis, B. G., Liberto, J. C. (1989). Metacognitive Strategy Training for ESL Reading. *TESOL Quarterly 23*, 647–678.

Castellino, A. R., Schuster, P. M. (2002). Evaluation of Outcomes in Nursing Students Using Clinical Concept Map Care Plans. *Nurse Educator, 27*, 149–150.
Carrell, P. L., Pharis, B. G., Liberto, J. C. (1989). Metacognitive Strategy Training for ESL Reading. *TESOL Quarterly 23*, 647–678.
Croasdell, D. T., Freeman, L. A., & Urbaczewski, A. (2003). Concept Maps for Teaching and Assessment. *Communications of the Association for Information Systems, 12*, 396-405.

Cook, V. (2001). Second Language Learning and Language Teaching. London: Hodder Education.

Cook, L. J. (2017). Using Concept Maps to Monitor Knowledge Structure Changes in a Science Classroom. Dissertations. 3139.

Daley, B. J., Shaw, C. R., Balistrieri, T., Glasenapp, K., Piacentine, L. (1999). Concept Maps: A Strategy to Teach and Evaluate Critical Thinking. *Journal of Nursing Education, 38*, 42–47.

Eppler, M. J. (2006). A Comparison between Concept Maps, Mind Maps, Conceptual Diagrams and Visual Metaphors as Complementary Tools for Knowledge Construction and Sharing. *Information Visualization,5*, 202 – 210.

Ertürk, Z. O. (2016). The Effect of Glossing On EFL Learners' Incidental Vocabulary Learning in Reading. *Procedia - Social And Behavioral Sciences*, 232(4), 373–381.

Fraser, K.M. (1993). *Theory Based Use of Concept Mapping in Organization Development: Creating Shared Understanding As A Basis for the Cooperative Design of Work Changes and Changes in Working Relationships*. Cornell University.

Graves, M. F. (2006). *The Vocabulary Book: Learning & Instruction.* Newark, DE: International Reading Association.

Harpaz, I., Balik, C., Ehrenfeld, M. (2004). Concept Mapping: An Educational Strategy for Advancing Nursing Education. *Nursing Forum, 39*, 27–30, 36.

Hart, B., & Risley, T. R. (1995). Meaningful Differences in the Everyday Experience of Young American Children. Baltimore, MD: Paul H. Brookes.

Irez, S., & Han, Ç. (2011). Utilizing Kuhnian Lenses For a Better Understanding of the Meaning of, and Resistance to, Educational Change. *International Journal of Environmental and Science Education*, 6(3), 251-266.

Laufer, B. (1997). The Lexical Plight in Second Language Reading. Cambridge: Cambridge University Press.

Liu, P. L., Chen, C. J., & Chang, Y. J. (2010). Effects of a Computer Assisted Concept Mapping Learning Strategy on EFL College Students' English Reading Comprehension. *Computers & Education, 54* (2010), 436–445.

Jia, Q. (2010). Abrief Study on the Implication of Constructivism Teaching Theory on Classroom Teaching Reform in Basic Education. *Journal of Educational Research*, 3(2), 197-199.

Jibrin, A., & Zayum, D. (2012). Effectiveness of Concept Mapping Strategy on Accadenic Achievement of Senior Secondary School Students in Genetics. *Journal of Science, Technology And Education, 1(1), 1- 53.*

Kathol, D. D., Geiger, M. L., Hartig, J. L. (1998). Clinical Correlation Map. A Tool for Linking Theory and Practice. *Nurse Educator, 23*, 31–34.

King, M., Shell, R. (2002). Critical Thinking Strategies. Teaching and Evaluating Critical Thinking With Concept Maps. *Nurse Educator, 27*(5), 214–21.

Kokkonen, T. (2017). Concepts and Concept Learning in Physics (Unpublished Doectoral Disertation). University of Helsinki, Helsinki.

Msanjila, Y. P. (1990). 'The Role and Status of Ethenic Languages in Tanzania. In *Kiswahili*: 57:46-54.

National Institute for Literacy. (2001). Put Reading First: The Research Building Blocks for Teaching Children to Read. Jessup, MD: National Institute for Literacy.

Novak, J. D., & Gowin, B. (1984). *Learning How To Learn*. Oxford: Cambridge University Press.

Ojima, M. (2006). Concept Mapping as Pre-Task Planning: A Case Study of Three Japanese ESL Writers. *Science Direct. System, 34* (2006), 566–585.

Richards, I. C., & Rodgers, T. S. (2001). Approaches and Methods in Language Teaching. Cambridge: Cambridge University Press.

Rupley, W. H., Logan, J. W., & Nichols, W. D. (1998/1999). Vocabulary Instruction in a Balanced Reading Program. The Reading Teacher, 52 (4).

Souleyman, H. M. (2009). Implicit And Explicit Vocabulary Acquisition with Computer Assisted Hypertext Reading Task: Comprehension and Retention. ARIZONA: University ff Arizona.

Stoica, I., Moraru, S., & Miron, C. (2011). Concept Maps, A Must for the Modern Teaching-Learning Process. *International Journal of Science Education*, 63(2), 567- 576.

Tarkashvand, Z. (2015). Male Learner's Vocabulary Achievement through Concept-Mapping and Mind Mapping: Differences And Simmilarities. Academic Journals, 790-798.

Wheeldon, J., & Faubert, J. (2009). Framing Experience: Concept Maps, Mind Maps and Data Collection in Qualitative Research. *International Journal of Qualitative Methods,* 8(3), 68-83.